



Mzozo wa Kifamilia na Visa ya Wapenzi

Wamiliki wa Visa ya Wapenzi si lazima wabaki katika uhusiano wa kuteswa ili kuendelea kuishi Australia.

Nchini Australia, mzozo wa kinyumbani na kifamilia haukubaliki.

Mpenzi, ndugu wa familia au watu wengine katika jamii hawawezi kutishia hali ya visa yako.

Kama unamiliki visa ya Mpenzi ya muda (Aina, 309 au 820) au Visa ya Ndoa Tarajiwa (aina 300) na unapitia mzozo wa kifamilia na uhusiano wako umeisha, kuna matoleo ndani ya sheria za uhamiaji za Australia za As above comment kukuruhusu kuendelea na maombi ya viza ya kudumu ya Mpenzi (Aina 100 au 801).

Ikiwa wewe au mtu unayemjua yuko hatarini, piga simu kwa polisi, nambari ya simu **000**.

Polisi nchini Australia ni salama na wanaweza kuaminika.

Kwa ushauri na maelezo ya bila malipo na ya siri, piga simu kwa 1800RESPECT, nambari ya simu **1800 737 732**.

Ikiwa unahitaji mkalimani bila malipo piga simu kwa **131 450**.

Australian Government (Serikali ya Australia) haivumilii mzozo wa kinyumbani na wa kifamilia katika hali yoyote ile.

Mzozo wa kinyumbani na wa kifamilia ni uhalifu dhidi ya sheria. Mtu anayetokeleza mzozo wa kinyumbani na wa kifamilia anaweza kwenda jela, awe ni mwanamume au mwanamke.

Mzozo wa kinyumbani ni tabia au vitisho ambavyo vina lengo la kumdhibiti mpenzi na kusababisha hofu kwa ajili ya usalama au ustawi.

Mtu yeyote anayepitia mzozo wa kinyumbani na wa kifamilia nchini Australia anaweza kupata msaada kutoka kwa huduma za misaada.

Unaweza kupata msaada haijalishi hali yako ya visa au ya uhamiaji.

Haijalishi kama uhusiano umemalizika au la - bado unaweza kupata msaada.

1800RESPECT ni huduma ya ushauri wa mzozo wa kijinsia, uhasama wa kifamilia na kinyumbani kutoka kwa taifa la Australia (Australia's national sexual assault, family and domestic violence counselling service). Hutoa maelezo na ushauri wa mtandaoni na wa simu bila malipo na wa siri. Washauri watakusikiliza, watajibu maswali na kukuelekeza kwa huduma nyingine za msaada katika eneo lako.

Piga simu kwa **1800 737 732** au nenda kwenye **tovuti ya 1800RESPECT** kwenye **www.1800RESPECT.org.au**.

Je unahitaji mkalimani?

Piga simu kwa **Huduma ya Ufasiri na Ukalimani (Translating and Interpreting Service (TIS))**, nambari ya simu **131 450**. Mkalimani kutoka TIS anaweza kukusaidia kuwasiliana na huduma zingine, hata hivyo TIS haitoi huduma ya ushauri. Simu zote hazilipishwi na ni za siri.

Kwa maelezo zaidi kuhusu mzozo wa kifamilia ikiwa una visa:

Maelezo ya ziada kuhusu mzozo wa kifamilia na visa yako kwenye tovuti ya Idara ya **Masuala ya Nyumbani (Department of Home Affairs)** kwenye **www.homeaffairs.gov.au**.